

MUHTASARI WA RIPOTI YA ALMA - ROBO YA 2, MWAKA 2026

“JUHUDI KUBWA YA KUHAJIKISHA TEKNOLOJIA MPYA ZINAWAFIKIA WANANCHI MAPEMA”

Utangulizi

Utafiti wa awali barani Afrika unaonesha kuwepo kwa pengo la takriban miaka mitano au zaidi toka pale teknolojia mpya ya tiba inapoanzishwa na hadi inapoanza kutumika katika nchi za Afrika, bila kujali idadi ya maisha yanayoweza kuokolewa.

Wakati Profesa Dkt. Corine Ngufor kutoka Benin alipoongoza majaribio ya kutumia vibanda maalum na tathmini za ki-entomolojia; au wakati Franklin W. Mosha na Dkt. Jacklin F. Mosha kutoka Tanzania walipoongoza majaribio muhimu yaliyodhibitiwa na kugawanywa katika makundi (cluster randomized controlled trials) kuhusu vyandarua vilivyotiwa dawa ya kuua wadudu yenye viambato aina mbili; wanasayansi hawa wa Kiafrika walikuwa na maono ya pamoja na walitaka kushughulikia tatizo la usugu wa viuatilifu kwenye vyandarua, kwa kutoa ushahidi wa majaribio ya tafiti ili kusaidia kutengeneza kizazi kijacho cha vyandarua; lengo likiwa ni kutoa kinga imara zaidi dhidi ya malaria kwa watoto, akina mama na familia barani Afrika haraka iwezekanavyo. Vyandarua hivi vyenye viambato aina mbili vina ufanisi mkubwa kwa takriban asilimia 45 zaidi kuliko vile vyenye kiambato kimoja (pyrethroid pekee).

Mbu walianza kuonesha usugu dhidi ya dawa ya kuua wadudu aina ya *pyrethroid* inayotumiwa kwenye vyandarua vilivyotiwa dawa kwa zaidi ya miaka 15 iliyopita, na mchango wa wanasayansi wa Kiafrika ulikuwa muhimu sana katika kuviwezesha vyandarua vyenye mchanganyiko wa viambato aina mbili kuwa tayari kuingia sokoni na kuilinda jamii.

Vyandarua aina mbili za kwanza zenye viambato viwili (Interceptor G2 na PermaNet Dual), vilipitishwa awali mnamo mwezi Machi 2023. Pamoja na kuwa vyandarua venye viuatilifu aina hizo mbili zilipendekezwa na Shirika la Afya Duniani kwa miaka mitatu iliyopita, bado kuna nchi zaidi ya kumi barani Afrika ambapo zaidi ya asilimia 20 ya vyandarua vyao ni vile zisivyofanya kazi vizuri.

Asilimia ya udhibiti wa vekta kwa mwaka uliopita kwa kutumia vifaa vya kizazi kipya




Chanzo: Robo ya 2, 2026 Kadi ya Alama ya Tathmini na Uwajibikaji ya ALMA
Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna
uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya
kisheria ya nchi yoyote, eneo au eneo la mamlaka yake au kuhusu
uwekaji mipaka au mipaka yake.

NCHI WANACHAMA

Algeria
Angola
Benin
Botswana
Burkina Faso
Burundi
Cameroon
Afrika ya Kati
Cabo Verde
Chad
Comoros
Jamhuri ya Congo
Côte d'Ivoire
Jamhuri ya
Kidemokrasia ya
Congo
Djibouti
Misri
Equatorial Guinea
Eritrea
Eswatini
Ethiopia
Gabon
Ghana
Guinea
Guinea Bissau
Kenya
Lesotho
Liberia
Libya
Madagascar
Malawi
Mali
Mauritania
Mauritius
Msumbiji
Morocco
Namibia
Niger
Nigeria
Rwanda
Jamhuri ya Sahrawi
Arab
Jamhuri ya São
Tomé na Príncipe
Senegal
Seychelles
Sierra Leone
Somalia
Afrika Kusini
Sudani Kusini
Sudan
The Gambia
Togo
Tunisia
Uganda
Jamhuri ya
Muungano wa
Tanzania
Zambia
Zimbabwe

Juhudi hii kubwa inawataka na kuwawajibisha wadau wote ili kuhakikisha kuwa maambukizi ya malaria yanazuiwa na maisha yanaokolewa. Hii inajumuisha kupunguza muda uliopo kati ya hatua ya kukamilika kwa ubunifu na hatua za kuhakiki sifa zake, kuidhinishwa na mamlaka husika nchini, na hatimaye kuanza kutumika katika jamii zetu.


Utekelezaji unaendelea vizuri katika kupunguza visa vya malaria kwa angalau asilimia 75 ifikapo mwaka 2025 (ikilinganishwa na 2015)



Chanzo: Robo ya 2, 2026 Kadi ya Alama ya Tathmini na Uwajibikaji ya ALMA

Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo au eneo la mamlaka yake au kuhusu uwekaji mipaka au mipaka yake.

Utekelezaji unaendelea vizuri katika kupunguza vifo vya malaria kwa angalau asilimia 75 ifikapo mwaka 2025 (ikilinganishwa na 2015)



Chanzo: Robo ya 2, 2026 Kadi ya Alama ya Tathmini na Uwajibikaji ya ALMA

Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo au eneo la mamlaka yake au kuhusu uwekaji mipaka au mipaka yake.

Nchi nyingi za Afrika haziko katika mwenendo sahihi wa kupunguza kiwango cha maambukizi au vifo vya malaria ili kufikia malengo ya mwaka 2030. Hii lazima iwe kichocheo kikuu cha juhudi za dhati za kuhakikisha kuwa ubunifu unaletwa katika jamii haraka iwezekanavyo.


Pengo katika uthibitishaji wa sifa wa awali

Muda unaotumiwa na Shirika la Afya Duniani kutathmini bidhaa mpya za afya kwa ajili ya matumizi umechelewesha matumizi ya dawa na bidhaa nyingi za kimatibabu. Shirika la Afya Duniani linashughulikia suala hili kwa kuanzisha mabadiliko kadhaa ya kiutaratibu ili kukabiliana na ucheleweshaji huo. Shirika la Afya Duniani limeanzisha mifumo ya kufanya tathmini sambamba na kuoanisha sera, huku tathmini zikifanyika kwa wakati mmoja. Pia, taratibu za tathmini zilzorahisishwa na zile za usajili wa ushirikiano zimeanzishwa, hatua zinazoweza upatikanaji wa haraka wa bidhaa hizo katika ngazi ya nchi.

Ili kuendana na uzalishaji wa ndani, Shirika la Afya Duniani hutoa msaada wa kiufundi ili kuwajengea uwezo wa uzalishaji wa ndani, pamoja na kurahishisha michakato na kufanya marekebisho ya kimfumo. Viuatilifu vya kupulizia angani vilivyotengenezwa Nairobi na Kampuni ya SC Johnson viliidhinishwa mapema ndani ya miezi 9, na kukamilisha tathmini kabla ya ratiba ya Shirika la Afya Duniani ambayo huchukua miezi kumi na miwili. Viuatilifu vya kupulizia angani huziba pengo muhimu katika udhibiti wa vekta – gharama ndogo ya matengenezo, huilinda jamii kwa mwaka mzima ambapo ni muhimu sana hasa kwa watu wanaohama-hama, huathiriwa wakati wa mchana/jioni, na inapotokea migogoro ya kibinadamu.

Hatua ya upimaji inayofuata kwa Shirika la Afya Duniani itakuwa ni mchakato wa awali wa kuidhinisha dawa mseto ya Ganlum (ganaplacide/lumefantrine) isiyotokana na artemisinin ambayo hutolewa kwenye pakiti ya punje na kunywewa mara moja kwa siku kwa muda wa siku tatu; dawa hii ilitengenezwa na kampuni ya Novartis pamoja na Shirika la MMV, ikiwa na kiwango cha ufanisi wa kutibu cha kati ya asilimia 97.4 hadi asilimia 99.2, na ilibuniwa ili kukabiliana na usugu dhidi ya dawa za artemisinin.

Utafiti kwenye ufanisi wa dawa uliofanywa tangu mwaka 2019 na takwimu kuripotiwa Shirika la Afya Duniani.



Chanzo: Robo ya 2, 2026 Kadi ya Alama ya Tathmini na Uwajibikaji ya ALMA
Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo au eneo la mamlaka yake au kuhusu uwekaji mipaka au mipaka yake.

Mchakato wa haraka wa kuhakiki sifa, kupata kibali cha kisheria na kuanza kutumika kwa dawa kutasaidia kudhibiti tatizo la usugu dhidi ya artemisinin, ambalo linaingia kimyakimya katika jamii zetu bila kufuatiliwa katika nchi 25.

Pengo katika Udhibiti


Usajili wa kawaida wa kitaifa kwa bidhaa zilizohakikiwa awali huchukua wastani wa miezi 12 hadi miezi 48. Nchi chache za Afrika zinashughulikia suala hili kwa ufanisi ili kuharakisha mchakato huo. Mfano unaofaa ni Ethiopia, nchi ambayo inachangia sehemu kubwa (zaidi ya asilimia 95) ya visa vyote vilivyoripotiwa vya malaria (*P. vivax*) katika Kanda ya Afrika ya Shirika la Afya Duniani.

Wakati dawa ya Tafenoquine yenye dozi moja kwa ajili ya malaria (*P. vivax*) ilipohakikiwa awali mnamo mwezi Desemba 2024, Mamlaka ya Chakula na Dawa ya Ethiopia (EFDA) ilikuwa tayari imeshasajili dawa hiyo tangu mwezi Juni 2023, kufuatia matokeo chanya ya majaribio yaliyofanyika nchini humo.

Shirika la Dawa la Afrika (AMA) sasa limekabidhiwa jukumu la kuunganisha juhudi mbalimbali zinazofanyika kote barani Afrika, ili kuoanisha mifumo ya udhibiti, kwa lengo la kuhakikisha;

- Kunakuwa na tathmini ya pamoja barani Afrika na kuorodhesha bidhaa katika kitabu cha kijani ili kusajili katika Daftari la Barani Afrika la Bidhaa zilizoorodheshwa.
- Mifumo ya kutegemeana kati ya mamlaka za udhibiti za kitaifa na Shirika la Afya Duniani, ili kuondoa mapitio ya ziada ya hati.
- Miongozo ya kiufundi iliyooanishwa kwa kushirikiana na kanda za kiuchumi.
- Usimamizi wa pamoja wa majaribio ya kimatibabu.
- Kudhibiti ubora na mtandao wa maabara wa vituo vya umahiri vya kikanda na maabara za kitaifa za udhibiti ubora.

Kutia saini, kuridhia na kuwasilisha Hati ya AMA katika AUC



Chanzo: Robo ya 2, 2026 Kadi ya Alama ya Tathmini na Uwajibikaji ya ALMA
Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo au eneo la mamlaka yake au kuhusu uwekaji mipaka au mipaka yake.

Nchi zinahimizwa kutia saini, kuridhia na kuwasilisha rasmi nyaraka za AMA, ili kuhakikisha kuwa Afrika nzima inatumia fursa hii kuokoa maisha ya Waafrika. Kwa sasa, nchi 16 hazijatia saini, na nchi 7 zimetia saini lakini hazijaridhia.

Hitimisho:

Mapambano dhidi ya malaria hayatafanikiwa bila uvumbuzi, utafiti na maendeleo ya teknolojia mpya. Wanasayansi wa Kiafrika wanashiriki katika juhudi hizi kubwa, wanapiga hatua na kuwa kichocheo cha mabadiliko ya kisayansi na uvumbuzi tunaohitaji. Wanasayansi wetu wako mstari wa mbele katika utafiti wenye kuleta mabadiliko makubwa ambao unaweza kuharakisha juhudi kuelekea kutokomeza kabisa malaria, kwa mfano, mbu wa kichocheo-jeni pamoja na chanjo mpya za malaria zenye kuleta mabadiliko makubwa.

Hata hivyo, zana hizi muhimu zinaweza kutokomeza kabisa malaria pale tu zitakapoletwa na kusambazwa katika jamii. Ni wakati muafaka wa kukomesha ucheleweshaji huu. Kila siku, tunapoteza watoto 1,200 walio chini ya umri wa miaka mitano, watoto 300 wanazaliwa wakiwa wamefariki, na wanawake wajawazito 35 wanaofariki dunia kutokana na malaria. Kote barani, watu 730,000 huambukizwa malaria kila siku, jambo linalosababisha madhara makubwa, ikiwemo kudorora kwa ukuaji wa akili, kupungua kwa uwezo wa kujifunza kwa wanafunzi, uzalishaji mdogo wa chakula, na kuongezeka kwa kutohudhuria kazini kwenye sekta muhimu.

Hii ndiyo gharama ya maisha na uhai kwa kila siku tunayochelewesha kuanzishwa kwa zana mpya zinazoweza kuzuia maambukizi, kuwezesha matibabu ya mapema ya malaria, na kuokoa maisha.

Ni wakati muafaka kwa wadau wote kuwajibishwa. Juhudi kubwa zinazofanywa zinalenga kuleta ufanisi na tija, pamoja na kuokoa maisha ili kuchochea ukuaji na maendeleo. Hii ndiyo njia pekee itakayotuongoza ili kufikia lengo la kutokomeza kabisa malaria.